**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Kwa:** Benki Zote,
Taasisi za Fedha,
Watoa huduma za Fedha kupitia mifumo ya simu za mkononi,
Watoa Huduma za Fedha kwa Njia ya Kielektroniki, na
Kampuni za Teknolojia ya Fedha.

## TAARIFA RASMI

## KUSHIRIKI KATIKA MAZINGIRA YA MAJARIBIO YA TEKNOLOJIA YA FEDHA YANAYODHIBITIWA NA BENKI KUU YA TANZANIA AWAMU YA PILI

---

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kutoa taarifa rasmi ya kufunguliwa kwa dirisha la maombi kwa awamu ya pili ili uweze kushiriki katika mazingira ya majaribio ya teknolojia ya fedha yanayodhibitiwa na Benki Kuu ya Tanzania.

Kampuni za Teknolojia ya Fedha na watoa huduma za fedha wenye nia ya kushiriki wanakaribishwa kuwasilisha maombi yao kupitia Tovuti ya kutuma maombi ya kushiriki katika mazingira ya majaribio ya teknolojia ya fedha yanayodhibitiwa na Benki Kuu ya Tanzania, kwa kuzingatia Kanuni za Udhibiti wa Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha za Mwaka 2024.

Dirisha la maombi kwa awamu ya pili limefunguliwa rasmi na litafungwa siku ya **Alhamisi, tarehe 23 Octoba, 2025**. Ili kuwasilisha maombi haya, tembelea tovuti hii: https://frsp.bot.go.tz/ na ujaze fomu ya maombi kwa njia ya mtandao. Mwongozo wa kina na vigezo vya kushiriki vinapatikana kwenye tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania.



2 Mtaa wa Mirambo, S. L. P. 2939, 11884 Dar es Salaam – Tanzania
Barua Pepe: DG-FSD-OFFICE@bot.go.tz Tovuti: www.bot.go.tz, Simu: +255 22 223 2000/3000/3215
Simu ya Mezani: +255 22 223 3045/3046

Bidhaa au huduma za fedha ambazo hazisimamiwi na sheria za Benki Kuu ya Tanzania pekee ndizo zitakazopokelewa kushiriki katika mazingira ya majaribio ya teknolojia ya fedha yaliyodhibitiwa.

Benki Kuu ina haki ya kuchapisha taarifa muhimu kuhusu waombaji katika tovuti yake, kwa madhumuni ya kuhamasisha ushirikiano wa kimataifa na kubadilishana maarifa na taasisi nyingine za udhibiti duniani, bila kufichua taarifa yoyote ya haki miliki au haki miliki ya kiubunifu ya mwombaji.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na: Dkt. Sigsbert Rwiza kupitia namba ya simu ya mkononi: +255 713 998 593 au barua pepe: Sigsbert.rwiza@bot.go.tz, Bw. Given Mhema kupitia namba ya simu: +255 711 788 830 au barua pepe: Given.mhema@bot.go.tz na Bw. January Bura kupitia namba ya simu: +255 685 547 4952 au barua pepe: January.bura@bot.go.tz.

Sauda K. Msemo
**Naibu Gavana**
**Uthabiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha**

11 Septemba, 2025



2 Mtaa wa Mirambo, S. L. P. 2939, 11884 Dar es Salaam – Tanzania
Barua Pepe: DG-FSD-OFFICE@bot.go.tz Tovuti: www.bot.go.tz, Simu: +255 22 223 2000/3000/3215
Simu ya Mezani: +255 22 223 3045/3046